JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA MANYARA
HALMASHAURI YA MJI WA BABATI

SHULE YA SEKONDARI BABATI
S.L.P,126,
BABATI.

MAWASILIANO YAFANYIKE KUPITIA NAMBA ZIFUATAZO,
Tarehe………………………

- Mkuu wa shule …………0784417899/0625977566
- M/Mkuu wa Shule ……..0787 822838 & 0784293813
- Mwandamizi Taaluma …0687 440745
- Malezi …………………..0786171306
- Email. babatiday.ss@babatitc.go.tz


MZAZI/ MLEZI WA ………………………………………………………………………………......
S.L.P …………………...................................
……………………………..………………………………………..............

**YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BABATI DAY – MANYARA**

Hongera sana kwa kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Babati Day. Uchaguzi wako ni ushahidi wa juhudi, nidhamu na mafanikio yako ya kitaaluma. Tunakutakia maandalizi mema ya kuanza safari mpya ya elimu ya juu ya sekondari yenye malengo makubwa ya mafanikio, ubunifu na uwajibikaji Katika Mchepuo wa HGL/HKL/HGFa/HGLi Kwa Mwaka……...

**Soma kwa makini taarifa na maelekezo ya kujiunga na shule kisha jaza fomu maalumu zilizoambatanishwa na kulipa michango yote kabla ya kuripoti shuleni.**

Napenda kukujulisha kuwa utapaswa kuripoti shuleni kuanzia tarehe…………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe………….. Kama hutofika mpaka tarehe…………… nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia saa 3:00 asubuhi  hadi saa 10:00 jioni siku za masomo.

Shule ipo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Babati kata ya Bagara kilometa 5 kutoka Stand kuu ya mabasi (Makatanini) na kilomita 0.5 kutoka mjini.

Namna ya kufika shuleni, anayetokea barabara ya Arusha shuka STAND KUU YA MABASI,kwa anayetoka barabara ya Dodoma shuka KONA YA MRARA AU MAHAKAMANI na anayetoka barabara ya Singida shuka TANESCO kisha ulizia Shule ya Sekondari Babati Day. NB; (stand kuu ya mabasi mpaka mjini nauli Tshs. 1,500/=, Mjini hadi shuleni nauli Tsh. 1,500/=.

Hii ni Shule ya Bweni na ni ya Wasichana tu.

## AIDHA UTAKAPOKUJA SHULENI LAZIMA UWE NA MAHITAJI YOTE YALIYOORODHESHWA HAPO CHINI.

### 1.1. MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE KWA MUHULA.

1. Mchango wa uendeshaji wa Shule ……………………………….65,000/=
2. Fedha za tahadhari ………………………………………………....5,000/=
3. Kitambulisho cha mwanafunzi na picha ni Tsh…………………....5,000/=
4. Nembo ya shule ni Tsh …………………………………………....5,000/=

**JUMLA KUU NI TSH……………………………………………………..80,000/=**

**N.B**. Malipo yote yanapaswa kufanyika katika Benki ya **NMB** kwa Akaunti Ifuatayo:- Babati day sekondari **A/C.No. 40701200117**. Unapaswa kuleta **Original Bank pay in slip** inayoonyesha jina la mwanafunzi, kidato na aina ya malipo **mfano:-** Mchango wa uendeshaji shule 65,000/= Tahadhari ni Tsh 5,000/= n.k (Hatutapokea fedha taslimu).

### 1:2. VIFAA VYA DARASANI.

1. Counter Book Quire 4 (Kubwa) 10
2. Mathematical set (DOMS/NATARAJ) tu.
3. Kalamu za wino na penseli.
4. Rula na kifutio.
5. Karatasi za photocopy (Ream 04($A_4$).
6. Picha nne (4) passport size za rangi za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu.
7. Scientific calculator(Non-Programable) kwa mwanafunzi wa jiografia.
8. **VITABU**: Vitabu ni rasilimali muhimu sana kwa mwanafunzi kwani humpatia maarifa kamili juu ya masomo yake mbalimbali kwa wakati husika. Shule ina vitabu vichache, na itaendelea kununua vitabu kulingana na kasma itolewayo na serikali kuhusu kifungu hicho. Kila mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mtoto wake angalau nakala chache za vitabu kulingana na uwezo alionao mzazi.

## ORODHA YA VITABU UNAVYO WEZA KUJINUNULIA.

### HISTORY

1. History for advance level form 5 Bakari madaya.
   - History for advance level form 6 by bakari madaya.
2. Advanced learning World History,By Idrisa Msuya,paper I and II.
   - History paper 2 notes
   - Advanced level F5 & F6
     By Gervas M. Zombe.
3. Advanced level History I and II by Shibitali C.K.Tumaini.
4. Medieval Ages paper I and II by M.Mavunde
5. History for Advanced level form 5 and 6. By TIE.

### ENGLISH

1. English Advanced Learners' Dictionary Seventh/ Sixth Edition By Oxford (waje na vitabu mtaala mpya ulioboreshwa)

### Novels (HGL&HKL)

1. Animal farm – George Orwel
2. Chasing the leopard finding Julie wake man lion.

3. The opportunist elite-Nyambari Nyangwine.
4. The horizon unveiled -Fellows Mwaisek.

## LIST OF PLAYS (HGLi).

1. Betrayal in the City – "Fancis Imbaga"
2. I will marry when I want "Ngung'o and Ngusi Wa Mirii"
3. Julius Caesar – William Shekespe
4. Man of kafia – Francis Imbuga.
5. A taste of heaven – Farouk tepan.

## POETRY (HGL&HKL)

1. Poets of African Boundless Vases poem.
2. The Bleeding heart from kenya Arthur of luck other poem and shuba keaya.
3. Summars poem from Tanzania -Richards Mabala.
4. Poets of Africa larcent of the silent and other poem- Jared Angira

## GEOGRAPHY

1. Physical Geography by TIE
2. Geography in Diagrams for Africa by R.B. Bunett
3. Practical Geography for Africa by TIE
4. Human & Economic Geography (Advanced level paper 2) by TIE
5. Map Reading for East Africa by D. N. McMaster
6. Practical Geography (Map, Photo, statistics, survey& Research) for A. Level by Zisti Kamili
7. Research Methology C.R.Kothari.
8. Principle of physical geography F.J Monkhouse.

## KISWAHILI

### VITABU - HKL

1. Kiswahili shule za sekondari kidato cha 5(muhtasari mpya) -kilangi enock lucas.
2. Kito cha lunga(sarufi,Tafsiri,Ukalimani na umahiri) -lubadanja E.E nyangani.
3. Kiswahili -Isimu kidatocha 5&6-Mwl.Jonas Leando kifunda
4. Kiswahili 1 Maswali na majibu kidato cha 5 na 6 -Samsoni Mahimbo Chacha
5. Umahiri katikaNadharia ya fasihi KISWAHILI 2-Samson Mahimbo Chacha
6. Tahakiki vitabu Teule vya fasihi kidato cha tano na sita -chacha S.m.

## GENERAL STUDIES

1. TIE (Form 5 & 6)
2. Alive General Studies form 5 & 6 by ZISTI KAMILI.
3. General Studies,form 5 & 6 by Maisha Mwaipaja.

**LITERATURE IN ENGLISH(HGLi)**

1. Arrow of god -Chinua Achebe.
2. A man of the people -Chinua Achebe.
3. A grain of wheat -Ngungi wa Thiongo.
4. Petals of Blood- Ngungi wa Thiongo.
5. No longer at easr – Chinua Achebe
6. Joy comes in the morning -Hoporang for Phororo.

7. The lion of yola -seven Nduguru.

## 1:3, VIFAA VYA USAFI NA VYOMBO VYA CHAKULA.

- Ndoo 2 za plastic za lita 20.
- Sabuni ya maji kwa ajili ya usafi wa vyoo lita 5.
- Toilet brush (mabrashi ya kusafisha vyoo – mafupi na
- Fagio za brashi laini za kufagilia ndani.
- Hard broom (brush ngumu ya kusugulia choo)
- Drying mopper (squeezer) ya kudekia.
- Kwanja-(HGL), Panga-(HKL) Jembe-(HGFa)-Reki-HGLi)
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

## 1:4, SARE YA SHULE:

Mzazi hakikisha mwanao ana:-

(i) Sketi mbili za kitambaa kizito rangi ya **DARK BLUE** Zenye mshono wa rinda box toka juu hadi chini mbele na nyuma na kulia na kushoto marinda madogo ya kawaida ) ziwe ndefu karibia na unyayo,Utajishonea mwenyewe.

(ii) Mashati ya rangi **NYEUPE** mawili ya mikono mirefu (Tetron), kwa wasichana wa kiislamu watavaa nusu kanzu ya rangi hiyo hiyo na kitambaa cha kichwani cha rangi hiyo hiyo **NYEUPE** chenye kufunika masikio na mabega (ushungi) usiwe na urembo -Utajishonea mwenyewe,asinunue tai.

(iii) Tai ndefu ya rangi ya **DARK BLUE** yenye mchirizi mweupe (**zitapatikana shuleni kwa tsh.5000/=**) kwa atakae hitaji kununulia shuleni

(iv) Sweta la rangi ya DARK BLUE lenye V. shape Shingoni,ajinunulie mwenyewe.

(v) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufungua kamba na vyenye visigino vifupi,aje navyo.

(vi) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe,aje nazo.

(vii) T - Shirt pana,ya rangi ya damu ya mzee (isiyo na maandishi) yenye kola(form six) (**Itapatikana shuleni kwa tsh.15000/= IKIWA NA NEMBO YA SHULE**) kwa watakao hitaji kununulia hapa shuleni.

(viii) Shamba dress sketi 1 kitambaa kizito rangi ya kahawia (brown) ya marinda ya kawaida ziwe ndefu karibia na unyayo,atajishonea mwenyewe.

(ix) Raba za michezo (zenye kamba) na soksi ndefu rangi ya blue (stockings),aje nazo

(x) Bukta na T-shirt (Jezi) ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo,aje nazo.

(xi) Tracksuit nzito za rangi NYEUSI zenye ufito mweupe pembeni mikononi na miguuni.

### Matandiko. (Ujinunulie)

xiv) Mashuka jozi 2 ya rangi ya light blue iliyoiva na pink iliyokolea na foronya zake.
xv) Mto (1)
xvi) Taulo
xvii) Kitenge au kanga 2 kwa ajili ya kuogea.
xviii) Nguo za ndani za kutosha
xix) Neti nyeupe Square '4 x 4'
xx) Godoro lenye 'cover' '2½ x 6'

***(MAGODORO YATABAKI SHULENI BAADA YAMWANAFUNZI KUMALIZA MASOMO YAKE KWAAJILI YA MATUMIZI YA SHULE)***

xxi) Blanket moja.
xxii) Sanduku la chuma lenye kufuli (Tranker)

## 1:5, SHERIA ZA SHULE.

### A: HESHIMA. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

1:5.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

  TUNASISITIZA WAZAZI WAWAKAGUE WATOTO WAO KABLA HAWAJAONDOKA NYUMBANI NA USIRUHUSU MWANAO AJE NA SIMU SHULENI.

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.Ruhusa hiyo itahusu - (Msiba wa mzazi/ndugu wa damu au Ugonjwa).

1:5.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MUHIMU (TANBIHI)**

Kila mwanafunzi aje na cheti halisi cha kuzaliwa na Kivuli chake (Photocopy) pamoja na hati ya matokeo (result slip).

**ZINGATIA:** Kila mwanafunzi aje na kadi ya **BIMA YA AFYA ya NHIF** ili kuepuka usumbufu kipindi cha maradhi,mwanafunzi hatapokelewa bila kuwa na huduma hii.Endapo mwanafunzi hana huduma ya Bima ya afya atapaswa kuja na Tsh.50,400/= ili utaratibu wa kupata bima ufanyike akiwa shuleni.

### 1.6 KUTEMBELEA WANAFUNZI

**Mzazi/mlezi aliyesajiliwa na mwenye picha katika faili la mwanafunzi ndiye atakayeruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa sababu maalum katika siku ya jumatatu hadi ijumaa ya wiki ya mwisho ya mwezi kuanzia saa 8:30 mchana hadi saa 9:30 alasiri.MAELEKEZO HAYA YAZINGATIWE NA WAZAZI.**

NB: **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ULIZOPEWA KWENYE FOMU HII NA SI VINGINEVYO.**

**VIAMBATANISHO MUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI.**

(i) Fomu ya mapokezi na utambulisho (joining instruction form).
(ii) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form).ijazwe katika Hospitali ya Serikali.
(iii) Cheti cha matokeo ya kidato cha nne(result slip)
(iv) Picha passport size 03 za wazazi au walezi watakaotambulika.
(v) Risiti za benki (pay in slip) kuonyesha malipo ya michango.

**MWISHO:** Ni matarajio yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii ya pekee uliyopewa na serikali na utakuwa mfano mzuri wa **KITAALUMA, NIDHAMU, KAZI, USAFI, NA MICHEZO.**

“Karibu sana Babati Day Sekondari, mahali ambapo maarifa, maadili na ufaulu hujengwa kwa pamoja kwa ajili ya kutimiza ndoto zako za baadaye.

Tunakuamini na tunatarajia kuona ukifanya vizuri zaidi katika masomo na maendeleo yako binafsi" (Discipline, Effort and Successess)

…………………

**MKUU WA SHULE**
**Simu Na:HM - 0784-417899 / 0625-977566**
Baruapepe. homaboa@gmai.com

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI WA BABATI**
**SHULE YA SEKONDARI BABATI.**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE.**
**FOMU HII IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI IKIWA IMEJAZWA KIKAMILIFU.**

**1. A: MWANAFUNZI.**

Mimi ……………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule yako, pia sheria zake za shule kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/ninakataa nafasi hiyo na masharti ya shule na sheria zake kwa sababu …………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

Tarehe ……………………………....  Sahihi …………………………

**B: MZAZI/MLEZI.**

Mimi ………………………………………………………………..Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… Ambaye amachaguliwa kujiunga na shule yako nimesoma maagizo na sheria zake. Ninakubali/ Ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha, naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kukuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.

Kama ninakataa (Eleza sababu) ……………………………………………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

Ahsante.

Jina na anuani ya Mzazi / Mlezi. ……………………………………………………
…………………………………………………………………………………

Sahihi ………………………………….. Tarehe ……………………………

(Futa lisilohusika).

NB: Sehemu 'B' Isainiwe na Mzazi/Mlezi na si vinginevyo.

**PRIME MINISTER'S OFFIC REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MANYARA REGION**
**BABATI TOWN COUNCIL**
**BABATI DAY SECONDARY SCHOOL**

**THE MEDICAL EXAMINATION FORM.**

*(To be completed by the Government Medical Officer and be returned to the school on registration day).*

Students name in full ……………………………………………………………

Blood count (Red and White Blood cells) ………………………………………

Stool Examination ………………………………………………………………

Urine analysis: …………………………………………………………………

Syphilis Test: ……………………………………………………………………

T.B. Test: ………………………………………………………………………

Ears: ………………………………………………………………………………

Chest: ………………………………………………………………………………

Spleen: ……………………………………………………………………………

Abdomen: …………………………………………………………………………

Pregnancy test……………………………………………………………………

Additional information e.g. physical Defects or Impairment infections, clinic or Family Diseases etc. ……………………………………………………………………

**DECLARATION:**

I certify that the above mentioned student is fit to pursue his/ her further studies.
(If do not fit please state it clearly)……………………………………………………

Doctors Name……………………………………………………………………………………

Doctor's signature……………………………………………………………………………

Date and Official Stamp…………………………………………………………………